JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

# TAARIFA YA UCHAGUZI WA MADIWANI, 1994

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

# TAARIFA YA UCHAGUZI WA MADIWANI, 1994

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

# TAARIFA YA UCHAGUZI WA MADIWANI, 1994

Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
26 Garden Avenue,
S.L.P. 10923,
Dar es Salaam, Tanzania.

Simu Na. 114963-6,
Telex Na. 41819,
Fax Na. 116740.

**TAARIFA YA UCHAGUZI WA MADIWANI, 1994**

# YALIYOMO

UKURASA


YALIYOMO .............................................. i

ORODHA YA VIAMBATISHO .............................. ii

1. MUHTASARI WA TAARIFA YA UCHAGUZI WA MADIWANI .......... 1

2. UTANGULIZI .............................................. 2

3. MAANDALIZI YA UCHAGUZI .............................. 4
   - 3.1 OFISI NA NYENZO ZA KUFANYIA KAZI .................. 4
   - 3.2 MAREKEBISHO YA SHERIA .............................. 5
   - 3.3 KUTANGAZA MAJINA NA MIPAKA YA KATA .............. 6
   - 3.4 MPANGO WA UTEKELEZAJI .............................. 7
   - 3.5 GHARAMA ZA UCHAGUZI WA MADIWANI .................. 7
   - 3.6 VIFAA VYA UCHAGUZI ................................. 9
   - 3.7 WATENDAJI ............................................ 10
   - 3.8. ELIMU YA UCHAGUZI KWA UMMA NA MAFUNZO KWA WATENDAJI WA SHUGHULI ZA UCHAGUZI ................ 11

4. UTEKELEZAJI .............................................. 14
   - 4.1 UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA ........................ 14
   - 4.2 UTEUZI WA WAGOMBEA ................................. 15
   - 4.3 PINGAMIZI .............................................. 19
   - 4.4 KAMPENI ZA UCHAGUZI ................................ 20
   - 4.5. UPIGAJI KURA ......................................... 22
   - 4.6 MATOKEO YA UCHAGUZI ................................ 24

5. HITIMISHO ................................................ 27

# ORODHA YA VIAMBATISHO


1. MPANGO WA UTEKELEZAJI ............................... 28

2. MAKADIRIO YA MATUMIZI YA UCHAGUZI WA MADIWANI, 1994 (REKEBISHO NA. 4) OKTOBA, 1994 ............................... 31

3. MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA UCHAGUZI ZILIZOTOLEWA NA WAHISANI MBALIMBALI ............................... 32

4. ORODHA YA VIFAA VILIVYOTUMIKA KATIKA UCHAGUZI WA MADIWANI ............................... 33

5. TAMKO LA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI JUU YA UCHAGUZI WA MADIWANI ............................... 35

6. KANUNI ZINAZOHUSU UTEUZI WA MADIWANI WA VITI MAALUM VYA WANAWAKE ............................... 36

7. ORODHA YA HALMASHAURI ZOTE TANZANIA BARA ZILIZOHUSIKA NA UCHAGUZI WA MADIWANI, OKTOBA, 1994 ............................... 38

# 1. MUHTASARI WA TAARIFA YA UCHAGUZI WA MADIWANI, 1994

1.1 Tume ya Taifa ya Uchaguzi ndiyo yenye mamlaka ya kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Uchaguzi wa Madiwani Tanzania Bara.

1.2 Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji 102 zenye jumla ya kata 2,411 zilishiriki kwenye uchaguzi uliofanyika tarehe 30 Oktoba, 1994. Halmashauri 94 ndizo zilizofanya uchaguzi. Hata hivyo, baadhi ya Kata za Halmashauri hizo hazikufanya uchaguzi kwa sababu wagombea wake walikuwa hawana wapinzani. Aidha, Kata zote za Halmashauri 8 hazikufanya uchaguzi kutokana na wagombea wa udiwani kupita bila kupingwa.

1.3 Fedha za kugharamia uchaguzi zilitolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na nchi wahisani za Denmark, Sweden, Jumuiya ya Ulaya (EEC), Marekani na Uingereza.

1.4 Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliandaa vifaa vya uchaguzi na vile vya elimu ya uchaguzi kwa umma na kuvipeleka kwa Wasimamizi wa Uchaguzi wa kila Halmashauri.

1.5 Uandikishaji wa wapiga kura ulifanyika tangu tarehe 1/8/1994 hadi 28/8/1994. Uteuzi wa wagombea ulikuwa tarehe 14/8/1994. Kampeni za uchaguzi zilianza tarehe 16/10/1994 hadi 29/10/1994. Siku ya uchaguzi ilikuwa tarehe 30/10/1994.

1.6 Aidha, kuhesabu kura kulifanyika tarehe 31/10/1994 na matokeo yalitangazwa mara baada ya zoezi la kuhesabu kura kukamilika. Jumla ya vyama 13 vya siasa vilishiriki uchaguzi kwa kusimamisha wagombea udiwani. Hata hivyo ni vyama 7 tu ndivyo ambavyo vilifanikiwa kupata viti vya udiwani. Vyama hivyo ni CCM, CHADEMA, NCCR-Mageuzi, UDP, CUF, UMD na TADEA.

# 2. UTANGULIZI

2.1 Mnamo tarehe tarehe 14 Januari, 1993, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano aliteua wajumbe wafuatao kuwa wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kwa mujibu wa Ibara ya 74(1), (2) na (3) ya Katiba ya Jamhuri ya mwaka 1977, na Kifungu cha 4 cha Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1985:

(a) Mhe. Jaji Lewis M. Makame,
Jaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania . . . . . . . . . . . . . . . . .Mwenyekiti

(b) Mhe. Jaji Augustino S. L. Ramadhani,
kutoka Zanzibar . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . Makamu Mwenyekiti

(c) Mhe. Ben Lobulu,
kutoka Chama cha Wanasheria (Tanganyika Law Society) . . . . . . Mjumbe

(d) Mhe. Mark D. Bomani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . Mjumbe

(e) Mhe. Solomon Liani . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . Mjumbe

(f) Mhe. Julie C. Manning . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . Mjumbe

(g) Mhe. Masauni Y. Masauni . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . Mjumbe

2.2 Pia tarehe 2 Machi, 1993, Rais alimteua Bw. Alex T. Banzi kuwa Mkurugenzi wa Uchaguzi. Kama Mkurugenzi wa Uchaguzi yeye ndie mtendaji mkuu wa Tume, na Katibu wa Tume, kwa mujibu wa Ibara ya 74(7) ya Katiba na Kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Uchaguzi, 1985.

2.3 Kwa mujibu wa Kifungu cha 12(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Chaguzi) Na. 4 ya mwaka 1979, Uchaguzi wa Kawaida wa Madiwani hufanyika kila baada ya miaka mitano katika kila Kata ya Mamlaka ya Serikali ya Mitaa (Halmashauri) Tanzania Bara.

2.4 Uchaguzi wa Madiwani wa mwaka 1994, ulifanyika baada ya Uchaguzi wa Madiwani wa mwaka 1988. Kufuatana na Sheria, uchaguzi huo ulitakiwa ufanyike mwaka 1993. Lakini kutokana na mabadiliko yaliyoifanya Tanzania kuwa na mfumo wa siasa wa vyama vingi kuanzia tarehe 1 Julai, 1992, uchaguzi huo uliahirishwa hadi tarehe 30 Oktoba, 1994.

2.5 Uchaguzi huo uliahirishwa kutokana pia na mamlaka ya kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Uchaguzi wa Madiwani kuhamishiwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Hapo awali uchaguzi huo ulisimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Hivyo Tume ilihitaji muda wa kufanya maandalizi ya uchaguzi huo.

2.6 Uchaguzi wa Madiwani wa mwaka 1994, ulikuwa ni uchaguzi wa kwanza wa madiwani, baada ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi, kufanyika katika mfumo huo mpya na kusimamiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

2.7 Madhumuni ya Taarifa hii ni kueleza kwa ufupi maandalizi na utekelezaji wa shughuli na hatua mbalimbali za uchaguzi huo wa Madiwani.

# 3. MAANDALIZI YA UCHAGUZI

## 3.1 OFISI NA NYENZO ZA KUFANYIA KAZI

3.1.1 Mara Tume ilipoteuliwa ilikabiliwa na matatizo makubwa kadhaa, yakiwemo ya ukosefu wa ofisi, ukosefu wa nyenzo za kufanyia kazi na uhaba mkubwa wa watendaji.

3.1.2 Kwa upande wa ofisi, Tume iliomba na kuazimwa vyumba viwili katika jengo la ofisi ndogo ya Bunge, Shaaban Robert Street, Dar e salaam. Siyo tu kwamba vyumba hivyo havikutosheleza hata ⅛ ya mahitaji ya Tume, lakini pia viliishusha sana hadhi ya Tume. Kwa upande mwingine Tume haikuona kwamba ni jambo jema kwa chombo hicho kuwamo katika jengo la Bunge. Jitihada za kuiomba Serikali iipatie Tume ofisi ziliendelea na hatimae, mnamo Machi, 1994, Serikali ilitoa jengo lake lililopo Na. 26 Garden Avenue, Dar es Salaam lililokuwa nyumba ya kuishi, litumike kama ofisi za Tume. Hata hivyo, jengo hilo nalo halikuweza kuanza kutumika hadi Desemba, 1994, kwa sababu:-

(a) Familia iliyokuwa inaishi humo haikuweza kuondoka mapema kutokana na ukosefu wa mahali pengine pa kuishi; na

(b) Lilihititaji marekebisho makubwa kabla ya kutumiwa kama ofisi.

3.1.3 Pia Tume ilikuwa haina ghala la kuhifadhia vifaa vya uchaguzi. Ni kweli kwamba ghala lililojulikana kama *Ivory Room* ndilo lililokuwa likitumiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kuhifadhia vifaa vya Uchaguzi wa Madiwani. Lakini ghala hilo lilikuwa likihifadhia pia vifaa vingine vya ofisi hiyo ambavyo si vya uchaguzi. Ongezeko la vifaa lililotokana na mfumo mpya wa uchaguzi ulifanya ghala hilo lisitoshe. Kwa sababu hizo Tume ililazimika kuazima maghala mawili kutoka Bohari Kuu ya Serikali kuhifadhia vifaa nyeti vya uchaguzi huo.

3.1.4 Kuhusu watumishi, kwa kipindi kirefu Tume iliwategemea maafisa wanne iliowaazima kutoka ofisi ya Bunge. Hatimae watumishi hao walihamishiwa Tume moja kwa moja na, kidogo kidogo Tume ilianza kupatiwa watumishi kutoka idara nyingine za Serikali.

3.1.5 Mbali na matatizo ya ofisi na watumishi, karibu katika kipindi chote cha Uchaguzi wa Madiwani kulikuwa na ukosefu na/au uhaba mkubwa wa vitendea

kazi. Kwa mfano Tume haikuwa na vifaa vya ofisi; simu, fax, wala telex yake yenyewe, na magari ya kuaminika.

3.1.6 Baadae ndipo:-

(a) Ubalozi wa Denmark uliipatia Tume magari sita yaliyokuwa yametumika kwenye mradi wa ujenzi wa barabara ya Chalinze - Segera; na

(b) Ubalozi wa Uingereza uliipatia Tume vifaa vya ofisi kama vile meza, viti, telexes, typewriters, duplicating machine, simu (switchboard and extensions), computers na photocopier. Hata hivyo haikuwezekana kutumia vifaa hivyo kabla ya kumalizika kwa Uchaguzi wa Madiwani. Kwa sababu utengenezaji wa jengo tulilopewa kama ofisi ulichukua muda mrefu na hatukuwa na mahali pengine pa kuviweka.

3.1.7 Kwa ujumla maandalizi ya Uchaguzi wa Madiwani yalifanyika katika mazingira magumu sana kutokana na sababu zilizotajwa hapo juu.

## 3.2 MAREKEBISHO YA SHERIA

3.2.1 Tanzania iliingia rasmi katika mfumo wa siasa wa vyama vingi kuanzia tarehe 1 Julai, 1992, kutokana na Sheria ya Mabadiliko ya Nane katika Katiba ya Nchi (Sheria Na. 4 ya mwaka 1992). Kufuatia hatua hiyo marekebisho ya kimsingi yalifanyika katika sheria mbalimbali, zikiwemo Sheria ya Serikali za Mitaa (Chaguzi) Na. 4/79, ambayo ilirekebishwa kwa Sheria Na. 7 ya mwaka 1992. Pia Sheria Na. 8 ya mwaka 1992, ilirekebisha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Na. 7 ya mwaka 1982, na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Na. 8/1982. Marekebisho hayo yote yalikuwa na madhumini ya:

(a) Kuondoa, katika Sheria za Uchaguzi wa Madiwani mambo yanayoambatana na uchaguzi katika mfumo wa chama kimoja cha siasa; na

(b) Kuweka katika Sheria za Uchaguzi wa Madiwani mambo ya kimsingi yanayoambatana na mfumo wa uchaguzi wa vyama vingi vya siasa.

3.2.2 Kama ilivyokwisha kudokezwa hadi wakati huo Uchaguzi wa Madiwani ulikuwa ukisimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais. Hata hivyo, tarehe 3 Machi, 1993, aliyekuwa Waziri wa Nchi (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) aliifahamisha Tume kwamba uchaguzi huo utasimamiwa na Tume na kwamba Bunge lilikwisha kupitisha mnamo Februari, 1993, Sheria Na. 1 ya mwaka 1993, ambayo:-

(a) Ilitoa tafsiri ya "Electoral Authority" katika Kifungu cha 2 cha Sheria Na. 4/79 kuwa na maana ya "National Electoral Commission"; na

(b) Ilifuta Kifungu chote cha 6 cha Sheria Na. 4/79 kilichohusu uundaji wa Mamlaka za Uchaguzi za Mikoa.

3.2.3 Tume ilimshauri Mheshimiwa Waziri kwamba kwa kuwa majukumu ya Tume yamewekwa na Katiba ni muhimu Ibara inayohusika, katika Katiba (74(6)), nayo irekebishwe ili kazi ya kusimamia na kuratibu uendeshaji wa Uchaguzi wa Madiwani ionyeshwe kuwa ni mojawapo ya majukumu ya Tume. Rekebisho hilo lilifanywa kwa Sheria Na. 7 ya mwaka 1993, (Sheria ya Mabadiliko ya Kumi Katika Katiba ya Nchi).

3.2.4 Pia Bunge lilipitisha Sheria Na. 4 ya mwaka 1993. Sheria hiyo ilirekebisha:-

(a) Sheria Na. 7 na Na. 8 za mwaka 1982, ili kuipa Tume ya Taifa ya Uchaguzi mamlaka ya kuweka utaratibu wa kuwachagua Madiwani wa viti maalum vya wanawake; na

(b) Sheria Na. 4/79 (Vifungu vya 9, 42, 58, 60, 63, 73, 109 na 125). Karibu marekebisho hayo yote yalitokana na mapendekezo ya Tume.

3.2.5 Vilevile kutokana na jukumu la kusimamia Uchaguzi wa Madiwani kuhamishiwa Tume, chombo hicho kiliomba uchaguzi huo uahirishwe kwa mwaka mmoja kwa sababu zifuatazo:-

(a) Ni muhimu Tume iwe kwanza na nyenzo za kutosha za kufanyia kazi;

(b) Kupata muda wa kufanya uchambuzi wa kina kuhusu marekebisho yanayohitajika katika sheria na taratibu mbalimbali za uchaguzi huo;

(c) Ni muhimu iwepo mipango ya kutosha ya kuwaelimisha wananchi juu ya demokrasia kwa jumla na hatimae juu ya hatua mbalimbali za uchaguzi; na

(d) Kuna mambo mengi ya utawala ambayo yanahitajika kuangaliwa kwa makini na kufanyiwa maamuzi ili kuleta ufanisi katika mazingira mapya ya uchaguzi wa vyama vingi, kwa mfano ruzuku na matumizi ya vyombo vya habari.

3.2.6 Marekebisho mengine yaliendelea kufanyika, hasa kwa Sheria Na. 11 ya mwaka 1994.

## 3.3 KUTANGAZA MAJINA NA MIPAKA YA KATA

3.3.1 Mwenye mamlaka ya kuunda Halmashauri na kuweka majina/mipaka ya Kata ni Waziri anayehusika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

3.3.2 Kwa ajili ya mipango sahihi ya shughuli za uchaguzi ilikuwa muhimu Tume izijue mapema sana Halmashauri zote pamoja na majina na mipaka ya Kata zake zote. Lakini Tume haikupatiwa orodha hiyo hadi Julai, 1994, yaani miezi mitatu tu kabla ya uchaguzi. Hata hivyo orodha hiyo ilikuwa na makosa mengi, na Halmashauri zinazohusika zilitoa masahihisho. Orodha hiyo ya majina ya Kata na mipaka yake ilitangazwa na Waziri katika Gazeti la Serikali la tarehe 15 Julai, 1994.

## 3.4 MPANGO WA UTEKELEZAJI

3.4.1 Ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli za Uchaguzi wa Madiwani, Tume iliandaa Mpango wa Utekelezaji (Action Plan) wa kipindi cha miezi 5 kuanzia mwezi Juni - Oktoba, 1994.

3.4.2 Mpango wa Utekelezaji ulikwenda sambamba na ratiba ya uchaguzi ambayo ilionyesha tarehe za matukio muhimu kama yalivyoainishwa hapa chini:-

(i) Uandikishaji wa Wapiga Kura tarehe 1/8/1994 - 14/8/1994. Baadae muda huo uliongezwa hadi tarehe 28/8/1994

(ii) Uteuzi wa Wagombea tarehe 7/8/1994. Baadae tarehe hiyo ilisogezwa mbele hadi tarehe 14 Agosti, 1994

(iii) Pingamizi Dhidi ya Uteuzi tarehe 8/8/1994

(iv) Kampeni za Uchaguzi tarehe 16.10.94 - 29.10.94

(v) Semina za Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura na Wasimamizi Wasaidizi tarehe 27.10.94 - 29.10.94

(vi) Siku ya Upigaji Kura tarehe 30.10.94

(vii) Kazi ya Kuhesabu Kura na Kutangaza Matokeo ilipangwa kufanyika kuanzia tarehe 31.10.94

3.4.3 Kwa ujumla Mpango wa Utekelezaji wa shughuli za uchaguzi pamoja na ratiba yenyewe ya uchaguzi ulizingatiwa ipasavyo. Nakala ya mpango wa utekelezaji imeambatishwa katika Taarifa hii kama Kiambatisho Na. 1.

## 3.5 GHARAMA ZA UCHAGUZI WA MADIWANI

3.5.1 Mpaka Tume ilipokabidhiwa shughuli za Uchaguzi wa Madiwani sehemu kubwa ya vifaa ilikwisha kununuliwa na ofisi ya Waziri Mkuu. Makadirio ya gharama za uchaguzi yaliyofanywa na Tume kwa ajili ya vifaa vilivyosalia na huduma nyinginezo yalifikia Shs. 9,053,622,400/=. Matumizi halisi yalikuwa pungufu (7,750,423,816/=) hasa kutokana na wagombea wa Kata 1,210 (kati ya Kata 2,411) kupita bila kupingwa na kufanya shughuli kadha kukomea njiani.

3.5.2 Makadirio hayo yaliyofanywa na Tume yalipelekwa Serikalini na pia kwa wahisani mbalimbali. Tarehe 18 Januari, 1994, na tarehe 9 Juni, 1994, Tume ilikutana na wahisani mbalimbali kuwaomba wasaidie kugharamia uchaguzi.

3.5.3 Katika mwaka wa fedha 1994/95, Serikali ilikubali kutoa Shs. 4,400,000,000/= lakini ilitoa Shs. 4,278,720,300/= kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| (a) | Awamu ya kwanza 28/7/94 | 2,122,000,000/= |
| (b) | Awamu ya pili 4/10/94 | 1,810,680,300/= |
| (c) | Awamu ya tatu 27/10/94 | 314,340,000/= |
| (d) | Awamu ya nne | 31,700,000/= |
| | | 4,278,720,300/= |

3.5.4 Kati ya fedha zilizotolewa na Serikali kiasi cha shilingi 3,932,680,300/= kilipelekwa kwa Wasimamizi wa Uchaguzi na Waratibu wa Uchaguzi wa Mikoa (Regional Local Government Officers) kwa ajili ya kuendesha uchaguzi. Fedha zilizotolewa na Serikali kiasi cha shilingi 346,040,000/= zilikuwa ni kwa ajili ya ruzuku kwa vyama vya siasa vilivyoshiriki katika uchaguzi.

3.5.5 Aidha mchanganuo wa makisio ya matumizi kwa Uchaguzi wa Madiwani, kiasi cha kutolewa na Serikali, na kiasi cha kuchangiwa na wahisani kimeonyeshwa katika Kiambatisho Na. 2.

3.5.6 Nchi na Jumuia mbalimbali za wahisani zilitoa shilingi 3,516,203,516 ili kugharimia uchaguzi kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| (a) | Denmark | 1,991,756,813/= |
| (b) | Sweden | 6,156,703/= |
| (c) | Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EEC) | 890,890,000/= |
| (d) | Marekani (USAID) | 11,700,000/= |
| (e) | Uingereza (UK) | 571,200,000/= |
| | | 3,471,703,516/= |

3.5.7 Kati ya fedha hizo zilizotolewa na wahisani, kiasi cha shilingi 656,590,000 kililipiwa vitu mbalimbali ambapo Uingereza ilitoa msaada wa kuchapisha karatasi za kura, kura bubu, kura maalum, na mfano wa karatasi ya kura (571,200,000/=), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EEC) (85,390,000/=) kwa ajili ya kununulia vifaa.

Mchanganuo wa matumizi mengine kwa fedha zilizotolewa na wahisani mbalimbali umeonyeshwa katika Kiambatisho Na. 3.

3.5.8 Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kupeleka fedha kwa Wasimamizi wa Uchaguzi ilizingatia idadi ya kata, idadi ya vituo na hata ukubwa wa Halmashauri.

## 3.6 VIFAA VYA UCHAGUZI

3.6.1 Vifaa vingi vya Uchaguzi wa Madiwani viliandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa mwanzoni uchaguzi huo ulikuwa unasimamiwa na ofisi hiyo. Hata hivyo Tume iliandaa vifaa vya elimu ya uchaguzi kwa umma, mishumaa, peni, *writing pads,* fomu za malalamiko (CF 3, 4, 5, 6 na 7). Fomu ya Taarifa (RF 1), fomu za uteuzi (Na. 2, 3, na 13), Tamko, Hadhari kwa Wapiga Kura, bahasha (Na. 1 - 5) masanduku ya kura, na kuchapisha karatasi za kura, kura bubu, mfano wa karatasi ya kura, na kura maalum. Tazama Kiambatisho Na. 4.

3.6.2 Tume iligawa vifaa vya uchaguzi kulingana na mahitaji ya kila Halmashauri. Baada ya mgao kukamilika vilisafirishwa katika awamu tatu kama ifuatavyo:-

(a) Vifaa vya uandikishaji wapiga kura vilisafirishwa katika awamu ya kwanza kwenda kwa Wasimamizi wa Uchaguzi wa kila Halmashauri mnamo mwezi Julai, 1994;

(b) Usafirishaji wa vifaa vya awamu ya pili ulihusu vifaa vya elimu ya uchaguzi kwa umma. Vifaa hivyo vilisafirishwa Agosti, 1994; na

(c) Mwanzoni mwa mwezi Oktoba, 1994, vilisafirishwa vifaa vya upigaji kura. Hiyo ilikuwa ni awamu ya tatu na ya mwisho ya usafirishaji wa vifaa vya uchaguzi kutoka makao makuu ya Tume.

3.6.3 Katika zoezi hilo, vyombo vya usafiri vilivyotumiwa ni ndege (ikiwemo ndege ya Serikali), meli, malori, mabasi, na magari ya baadhi ya Wasimamizi wa Uchaguzi ambao walikuwa wakija Dar es Salaam kwa shughuli zao.

3.6.4 Zoezi zima lilikuwa na mafanikio isipokuwa kwa baadhi ya Halmashauri ambako mvua na ubovu wa barabara vilisababisha kuchelewa kwa vifaa kuzifikia Halmashauri hizo. Kwa mfano, vifaa vya Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea, vilibaki Lindi Mjini.

3.6.5 Hata hivyo kwa jumla vifaa vyote vilifika vilikotarajiwa, kwa wakati muafaka, na idadi iliyoandaliwa ilitosheleza mahitaji.

## 3.7 WATENDAJI

3.7.1 Watendaji wa shughuli za Uchaguzi wa Madiwani huteuliwa kwa mujibu wa Sheria Na. 4/79. Wasimamizi wa Uchaguzi walioteuliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) cha Sheria hiyo, kutokana na nyadhifa zao katika Halmashauri, ni kama ifuatavyo:-

(a) Naibu Mkurugenzi wa Jiji
(b) Wakurugenzi wa Manispaa
(c) Wakurugenzi wa Miji
(d) Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya

Jumla ya Wasimamizi wa Uchaguzi ilikuwa 102.

3.7.2 Hata hivyo, chini ya Kifungu cha 9(6) cha Sheria Na. 4/79, Mkurugenzi wa Uchaguzi anaweza kuteua mtu mwingine kuwa Msimamizi wa Uchaguzi badala ya hao waliotajwa na sheria.

3.7.3 Kama ilivyo katika Sheria ya Uchaguzi wa Madiwani, Wasimamizi wa Uchaguzi ndio waliowateua Wasimamizi Wasaidizi. Pamoja na wengineo, kila Kata ilikuwa na Msimamizi Msaidizi mmoja.

3.7.4 Kwa mamlaka iliyopewa na Kifungu cha 10(1) cha Sheria Na. 4/79, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliwateua Wasimamizi wa Uchaguzi wote kuwa ndio pia Maafisa Waandishi (Registration Officers). Hao nao waliwateua Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi kuwa Maafisa Waandishi Wasaidizi (Assistant Registration Officers).

3.7.5 Kwa ajili ya zoezi la kuandikisha wapiga kura, Maafisa Waandishi ndio waliokuwa na mamlaka ya kuteua Waandishi Wasaidizi (Registration Assistants). Ili kwenda sambamba na mazingira ya uchaguzi katika mfumo wa vyama vingi, Tume ilitoa maelekezo yafuatayo kuhusu uteuzi wa Waandishi Wasaidizi:-

(a) Vyama vifahamishwe utaratibu utakaotumika;
(b) Maafisa Waandishi (wakisaidiwa na Maafisa Waandishi Wasaidizi) wateue majina (mengi kuliko mahitaji);
(c) Utangazaji wa majina hayo kwenye makao makuu ya Kata;

(d) Kuvipa nafasi vyama vilivyopata usajili kamili kutoa pingamizi, kama wanazo, dhidi ya jina lolote; na

(e) Kufanya uteuzi rasmi.

3.7.6 Utaratibu huo ulitumiwa pia na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi wakati wa kuteua Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura na Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo hivyo.

3.7.7 Wasimamizi wa Uchaguzi ndio waliowateua walinzi wa vituo vya kupigia kura. Uteuzi wa wahesabu kura ulifanywa na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi, ngazi ya Kata.

## 3.8 ELIMU YA UCHAGUZI KWA UMMA NA MAFUNZO KWA WATENDAJI WA SHUGHULI ZA UCHAGUZI

3.8.1 Tume iliandaa programu ya Elimu ya Uchaguzi kwa Umma. Katika progamu hiyo:-

(a) Yalitolewa maelekezo mbalimbali kwa watendaji, vyama, wagombea na wapiga kura;

(b) Kipindi cha Radio cha "Mnazi Mmoja" kilitayarishwa kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la nchi za nje la Uingereza (ODA);

(c) Zilitengenezwa kanga na fulana zenye ujumbe wa Uchaguzi wa Madiwani;

(d) Warsha ya siku moja juu ya nadharia na hali halisi inayohusu chaguzi za Serikali za mitaa iliandaliwa na Tume kwa msaada wa Shirika la Kijerumani liitwalo "Friedrich Ebert Stiftung". Warsha hiyo iliyofanyika Dar es Salaam tarehe 16 Desemba, 1993, ilihudhuriwa na:

(i) Wajumbe wote wa Tume, Mkurugenzi wa Uchaguzi na baadhi ya Maafisa waandamizi wa Tume; na

(ii) Wasomi na watu mbalimbali wenye uzoefu katika utawala na uendeshaji wa Serikali za Mitaa hapa Tanzania, miongoni mwao ni Prof. Baregu, Dr. Ngware na Dr. Halfan wote kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wengine ni Bwana F. Ndaba (Kamishna wa Serikali za Mitaa) na Bwana J. O. Max (aliyewahi pia kuwa Kamishna wa Serikali za Mitaa).

3.8.2 Katika warsha hiyo ya siku moja mada sita (6) zilitolewa nazo ni:

: Introduction to Local Government (C. A. Kallaghe);

: Attitude of the Central Government to Local Government (J. C. Kilembe);

: Some Features in Grassroot Elections (B. R. Nchimbi);

: Field Organisation and Mobilisation for Elections (J. Kitula);
: Rural Public Awareness of Elections (M. Ndikwege); na
: Problems of Urban Representation (G. P. Chale).

3.8.3 Tume ilitoa elimu ya uchaguzi kwa watendaji wa shughuli za uchaguzi, vyama vya siasa, wagombea na umma kwa ujumla kwa njia mbalimbali kama vile:-

(i) Kuandaa na kusambaza maelekezo kwa Wasimamizi wa Uchaguzi, Waandishi Wasaidizi, Wapiga Kura, Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura na Vyama vya Siasa na Wagombea;
(ii) Kutoa matangazo kwenye vyombo vya habari;
(iii) Kutengeneza na kusambaza vipeperushi (leaflets);
(iv) Kutengeneza na kusambaza mabango na *stickers*;
(v) Kutengeneza na kusambaza kanga, fulana; na
(vi) Kuandaa na kuendesha warsha/semina.

3.8.4 Tume, pia, iligharamia utoaji wa matangazo ya radio na kwenye magazeti ambayo yalielezea masuala muhimu na taratibu ambazo wapiga kura walitakiwa kuzifuata ili kufanikisha uchaguzi huo.

3.8.5 Kwa msaada wa Shirika la Maendeleo la nchi za nje la Uingereza (ODA), Tume, ilianzisha Kipindi cha Radio cha "Mnazi Mmoja", ambacho kilitoa elimu ya uchaguzi katika hatua zote za uchaguzi, yaani kuanzia kipindi cha uandikishaji wapiga kura hadi upigaji kura.

3.8.6 Warsha ya Waandishi wa vifaa vya elimu ya uchaguzi (writers workshop) ilifanyika katika Hoteli ya Kunduchi, Dar es Salaam, tangu tarehe 11 Juni, 1994, hadi tarehe 17 Juni, 1994. Madhumuni ya warsha hiyo ilikuwa:-

(a) Kutayarisha Maelekezo kwa Wasimamizi wa Uchaguzi, Wapiga Kura, Waandishi Wasaidizi, Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura na Vyama vya Siasa na Wagombea;
(b) Vipeperushi (leaflets); na
(c) Mabango (posters) na *stickers*.

Warsha hii iligharamiwa na Ubalozi wa Denmark.

3.8.7 Warsha ya Wakufunzi (Training of Trainers Workshop) ilifanyika Kibaha katika Mkoa wa Pwani, tangu tarehe 20 Juni, 1994, hadi tarehe 23 Juni, 1994. Madhumuni ya warsha hii yalikuwa ni kuwaandaa Wakufunzi ambao ndio watakaotoa mafunzo kwa Wasimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri zote za Tanzania Bara.

3.8.8 Semina za Wasimamizi wa Uchaguzi zilifanyika katika kanda tano tangu tarehe 27 Juni, 1994 hadi tarehe 29 Juni, 1994, kanda hizo ni:-

(a) Nyanda za Juu Kusini: Warsha ilifanyika mjini Mbeya na iliwajumuisha Wasimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri za mikoa ya Mbeya, Iringa, Ruvuma na Rukwa;

(b) Kati: Ilifanyika mjini Dodoma na ilijumuisha Wasimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri zilizo katika mikoa ya Dodoma, Tabora na Kigoma;

(c) Pwani na Kusini: Warsha ilifanyika mjini Morogoro na ilijumuisha Wasimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri zilizo katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Mtwara na Lindi;

(d) Ziwa: Warsha ilifanyika mjini Mwanza na kuwajumuisha Wasimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri zilizo katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara; na

(e) Kaskazini: Warsha ilifanyika mjini Moshi na ilijumuisha mikoa ya Singida, Arusha, Kilimanjaro na Tanga.

3.8.9 Semina za Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi na Waandishi Wasaidizi, ziliendeshwa na Wasimamizi wa Uchaguzi katika Halmashauri zao. Madhumuni ya semina hizo ilikuwa ni pamoja na:-

(a) Kuwaelimisha Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi juu ya usimamizi na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za uchaguzi katika ngazi ya Kata; na

(b) Kuwafundisha Waandishi Wasaidizi masuala muhimu ambayo walitakiwa kuyatekeleza wakati wa kuandikisha wapiga kura.

3.8.10 Semina za Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura ziliandaliwa na Wasimamizi wa Uchaguzi ili kuwapa maelekezo ya kisheria, taratibu za usimamizi wa vituo vya kupigia kura, kufunga vituo na masanduku ya kura. Semina hizi zilifanyika kati ya tarehe 27 Oktoba, 1994, hadi tarehe 29 Oktoba, 1994, Mawakala wa upigaji kura pia walishiriki semina hizo.

3.8.11 Tume pia ilitafsiri Sheria ya Serikali za Mitaa (Chaguzi) Na. 4 ya mwaka 1979, katika lugha ya Kiswahili kwa madhumuni ya kuelimisha umma. Uchapishaji wa nakala laki moja (100,000) wa tafsiri hiyo uligharamiwa na SIDA kwa niaba ya Serikali ya Sweden na kundi la wahisani kwa Shs. 6,156,703/=.

3.8.12 Tatizo lililojitokeza ni kuwa baadhi ya fedha za kutayarisha vifaa vya elimu ya uchaguzi kwa umma zilichelewa kutolewa na vifaa hivyo vikachelewa kuandaliwa na kusambazwa kwa wananchi.

# 4. UTEKELEZAJI

## 4.1 UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA

### 4.1.1 Idadi ya Wapiga Kura

Kwa mujibu wa Kifungu cha 15 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Chaguzi) Na. 4 ya 1979, kila raia mwenye umri wa miaka kumi na nane (18) au zaidi anayo haki ya kuandikishwa kupiga kura.

Tume ilikadiria kwamba watanzania wasiopungua 10,627,122 wangeandikishwa kupiga kura. Hata hivyo, watu walioandikishwa walikuwa 7,967,350. Idadi hii ni sawa na asilimia 77.4 ya makisio.

Uandikishaji wa wapiga kura katika Uchaguzi wa Madiwani wa mwaka 1994, ulianza tarehe 1 Agosti, 1994, na ulipangwa kumalizika tarehe 14 Agosti, 1994. Katika kipindi hiki ilionekana wazi kuwa idadi ya watu walioandikishwa ilikuwa ni ndogo mno kuliko ilivyokadiriwa. Kutokana na sababu hiyo, Tume ililazimika kuongeza muda wa uandikishaji wa wapiga kura kwa siku 14 zaidi, yaani, kuanzia tarehe 15 Agosti, 1994, hadi tarehe 28 Agosti, 1994. Lakini zoezi la kuandikisha wapiga kura katika Kata zilizokuwa na mgombea mmoja liliisha tarehe 14 Agosti, 1994, siku ile ya uteuzi. Kata hizo hazikuhusika na uandikishaji awamu ya pili.

4.1.2 Katika kipindi cha uandikishaji wa wapiga kura mambo yalikwenda kama ilivyopangwa isipokuwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Katika Halmashauri hiyo kulikuwapo na kutokuelewana na mizozo kuhusu malipo kati ya Msimamizi wa Uchaguzi na Waandishi Wasaidizi. Kutokana na hali hiyo baadhi ya Waandishi Wasaidizi waligoma na hawakuwenda kwenye vituo vya uandikishaji au walikwenda kwa nyakati walizopenda wenyewe.

4.1.3 Mzozo huo uliathiri shughuli zote za uandikishaji wa wapiga kura katika Halmashauri ya Jiji kwa namna tatu kama ifuatavyo:-

(a) Idadi kubwa ya wakazi wa Dar es Salaam waliotaka kuandikishwa walishindwa na hivyo kunyimwa bure haki yao ya kuandikishwa;

(b) Baadhi ya Waandishi Wasaidizi hao walivichukua vitabu vya kuandikishia wapiga kura na waligoma kuvirudisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi. Hivyo Msimamizi wa Uchaguzi hakuwa na kumbukumbu sahihi ya wale walioandikishwa; na

(c) Baadhi ya Waandishi Wasaidizi hao ambao hawakurejesha vitabu hivyo vya kuandikishia wapiga kura, waliviuza.

4.1.4 Kutokana na hitilafu hizo, Tume iliamua:-

(a) Kufuta uandikishaji wa awali kwa Halmashauri yote ya Jiji la Dar es Salaam na kufanya uandikishaji mpya kabisa kuanzia tarehe 26 Septemba, 1994, hadi 9 Oktoba, 1994;

(b) Kuwaachisha kazi Waandishi Wasaidizi waliohusika na kuandikisha katika awamu ya kwanza na kuajiri wengine wapya; na

(c) Kwa mujibu wa Kifungu cha 9(6) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Chaguzi) Na. 4 ya 1979, Tume ilimshauri Mkurugenzi wa Uchaguzi kumteua Mkurugenzi wa Jiji kuwa Msimamizi wa Uchaguzi badala ya Naibu Mkurugenzi wa Jiji kama inavyotajwa na Kifungu cha 9(1) cha Sheria hiyo.

4.1.5 Katika juhudi za kupanua na kuimarisha demokrasia nchini, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliamua kuvishirikisha vyama vya siasa katika zoezi la kuandikisha wapiga kura. Vyama vya siasa vilipewa nafasi ya kuteua wawakilishi wao katika kila kituo cha kuandikisha wapiga kura ili kuhakikisha kwamba uandikishaji wa wapiga kura unafanyika kwa uwazi.

4.1.6 Kulikuwa na tatizo la mawasiliano lililosababisha Tume kutopata takwimu sahihi za idadi ya watu walioandikishwa kutoka kwa Wasimamizi wa Uchaguzi. Tatizo hili lilisababisha Tume ishindwe kutoa mapema idadi ya karatasi za kura na kura bubu kwa mchapishaji. Pia fedha zilizotumwa kwa baadhi ya Halmashauri zilichelewa kufika kwa sababu ya tatizo la mawasiliano kati ya NBC Makao Makuu na matawi yake. Hali hiyo iliathiri zoezi la uandikishaji wapiga kura.

4.1.7 Pamoja na tatizo la mawasiliano na lile la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa ujumla zoezi la kuandikisha wapiga kura katika Uchaguzi wa Madiwani lilifanikiwa kwa kiwango cha kuridhisha. Kama ilivyokwisha kuelezwa, ni asilimia 77.4% ya watu waliotegemewa kuandikishwa waliweza kuandikishwa na zoezi zima la kuandikisha wapiga kura liliendeshwa kwa utulivu na amani.

## 4.2 UTEUZI WA WAGOMBEA

Uteuzi wa wagombea udiwani ulifanyika katika hatua mbili muhimu. Hatua ya kwanza ulikuwa ni uteuzi ndani ya vyama vya siasa. Hatua ya pili ya uteuzi ilikuwa ule uliofanywa na Wasimamizi wa Uchaguzi.

4.2.1 Uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa ni kutimiza masharti ya Kifungu cha 39(2)(f) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Chaguzi) Na. 4/79 kuwa mgombea awe ni mwanachama wa chama cha siasa kilichopata usajili kamili

na awe amependekezwa na chama cha siasa kuwa mgombea. Uteuzi katika hatua hii uliathiri zoezi la upigaji kura kwa sababu baadhi ya wanachama wasioridhika na jinsi uteuzi huo ulivyofanyika ndani ya vyama vyao vya siasa walipeleka malalamiko yao mahakamani ambapo zilitolewa amri za kusimamisha uchaguzi wa Kata hizo. Kwa mfano uchaguzi wa Kata za Kigamboni (Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam) na Nyakatende (Halmashauri ya Wilaya ya Musoma), wanachama wa CCM walilalamika mahakamani kuwa demokrasia haikutumika kwenye uteuzi wa wagombea kwa tiketi ya chama chao. Mahakama ya Hakimu Mkazi Kivukoni na Mahakama ya Hakimu Mkazi Musoma zilitoa amri ya kusimamisha uchaguzi katika Kata hizo.

4.2.2 Wasimamizi wa Uchaguzi walishughulikia uteuzi wa wagombea kama walivyopendekezwa na vyama vya siasa na kwa kutimiza masharti ya uteuzi kama yalivyoainishwa chini ya Kifungu cha 39(2) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Chaguzi) Na. 4/7 ambayo ni:

(a) Awe ni raia wa Jamhuri ya Muungano.
(b) Amefikia umri wa miaka ishirini na moja (21).
(c) Hakukosa sifa ya uchaguzi chini ya Kifungu cha 40.
(d) Awe ni mkazi wa kawaida wa eneo lililo chini ya Serikali za Mitaa.
(e) Anaweza kusoma na kuandika kiswahili au kiingereza.
(f) Awe ni mwanachama wa chama cha siasa kilichopata usajili kamili na amependekezwa na chama cha siasa.
(g) Awe ana njia halali ya kujipatia riziki.
(h) Awe hadaiwi kodi yoyote.

4.2.3 Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitoa ufafanuzi kwa Wasimamizi wa Uchaguzi kuwa kodi inayohusika ni kodi ya maendeleo na sio kodi nyingine yoyote. Kama mgombea atakuwa hakulipa kodi ya maendeleo alichukuliwa kuwa hana sifa ya kugombea udiwani.

4.2.4 Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipanga tarehe 7 Agosti, 1994, kuwa ndiyo siku ya uteuzi. Vyama vya siasa viliwasilisha maombi ya kusogeza mbele siku ya uteuzi ili kutoa muda kwa wagombea kupata wadhamini kwa vile zoezi la uandikishaji lilikuwa linakwenda taratibu mno. Watu walioandikishwa kwa baadhi ya maeneo walikuwa hawatoshi kuwadhamini wagombea wa vyama vya siasa waliotaka kugombea udiwani. Tume ilikubaliana na ombi hilo na kusogeza uteuzi mbele kwa siku saba, yaani tarehe 14 Agosti, 1994. Hiyo ndiyo siku ambayo wagombea walioteuliwa na vyama vyao walitakiwa kuwasilisha rasmi fomu za uteuzi kwa Msimamizi wa Uchaguzi.

4.2.5 Tume iliamua na kuelekeza kwamba fomu hizo zirudishwe kwa Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata kwa vile kisheria, katika suala hilo nao wana mamlaka sawa kabisa na yale ya Wasimamizi wa Uchaguzi wenyewe.

4.2.6 Tarehe 14 Agosti, 1994, uteuzi ulifanyika katika Kata 2,406. Kata tano hazikufanya uteuzi kwa sababu hakuna wagombea waliorudisha fomu za uteuzi siku hiyo ya uteuzi. Kata hizo ni Lumbila (Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa), Wampembe (Halmashauri ya Wilaya ya Nkansi), Nanjilinji (Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa), Ilonga (Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga) na Ndumbwe (Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara). Tarehe mpya ya uteuzi iliyopangwa na Tume kwa Kata hizo isipokuwa Kata ya Lumbila, ilikuwa tarehe 28 Septemba, 1994.

Kata ya Lumbila haikufanya uteuzi kwa sababu ya tatizo la mawasiliano kati ya Tume na makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya.

4.2.7 Vyama vyote kumi na vitatu (13) vilivyopata usajili kamili vilishiriki. Chama kilichoshiriki katika Kata nyingi zaidi ni CCM ambacho kilishiriki katika Kata 2,409. Chama kilichoshiriki katika Kata chache zaidi ni UPDP ambacho kilishiriki katika Kata 12 tu. Kwa ujumla vyama vya siasa vilishiriki kama ifuatavyo:-

| JINA LA CHAMA | | IDADI YA WAGOMBEA |
|---|---|---|
| 1. | CCM | 2,409 |
| 2. | CHADEMA | 478 |
| 3. | CUF | 332 |
| 4. | UMD | 170 |
| 5. | UDP | 153 |
| 6. | TADEA | 52 |
| 7. | TLP | 41 |
| 8. | PONA | 39 |
| 9. | NCCR-MAGEUZI | 32 |
| 10. | TPP | 27 |
| 11. | NRA | 22 |
| 12. | NLD | 19 |
| 13. | UPDP | 12 |
| | | 4,078 |

4.2.8 Katika wagombea hao hapo juu, jumla ya wagombea 1,210 hawakuwa na wapinzani kama ifuatavyo:-

| JINA LA CHAMA | | IDADI YA KATA |
|---|---|---|
| 1. | CCM | 1,208 |
| 2. | UDP | 1 |
| 3. | NCCR-MAGEUZI | 1 |
| | | 1,210 |

4.2.9 Katika wagombea wa uchaguzi huo kulikuwa na wagombea wanawake hamsini na saba (57) tu wakiwa wameteuliwa na vyama vya:-

| JINA LA CHAMA | | IDADI YA WAGOMBEA |
|---|---|---|
| 1. | CCM | 26 |
| 2. | CHADEMA | 7 |
| 3. | UMD | 5 |
| 4. | TPP | 4 |
| 5. | NCCR MAGEUZI | 3 |
| 6. | TADEA | 3 |
| 7. | UDP | 3 |
| 8. | CUF | 2 |
| 9. | TLP | 1 |
| 10. | UPDP | 1 |
| 11. | NLD | 1 |
| 12. | NRA | 1 |
| | | 57 |

PONA haikuwa na mgombea mwanamke.

4.2.9 Wagombea wa CCM katika Kata za Melela (Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro), Njoro (Halmashauri ya Wilaya ya Same), Ruanda (Halmashauri ya Manispaa ya Mbeya), mgombea wa CHADEMA Kata ya Kirumba (Halmashauri ya Manispaa ya Mwanza) na mgombea wa NCCR-MAGEUZI Kata ya Kikuyu (Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma) walifariki dunia kabla ya uchaguzi, hivyo uteuzi ulirudiwa kwa mujibu wa Kifungu cha 51(2) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Chaguzi) Na. 4/79. Uteuzi mpya katika Kata hizo ulifanyika tarehe 28 Septemba, 1994.

4.2.10 Uteuzi katika Kata za Kashenye na Kanyigo (Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba Vijijini) ulitenguliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutokana na rufaa

zilizowasilishwa Tume dhidi ya uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi. Hivyo Tume ilitangaza tarehe mpya ya uteuzi kuwa tarehe 28 Septemba, 1994.

4.2.11 Tume ilitengua uteuzi wa wagombea udiwani katika Halmashauri yote ya Ngorongoro kutokana na Halmashauri hiyo kufanya uteuzi wa wagombea udiwani katika tarehe mbalimbali badala ya tarehe 14 Agosti, 1994. Tume ilipanga kuwa uteuzi mpya ufanyike tarehe 5 Oktoba, 1994.

## 4.3 PINGAMIZI

Kwa mujibu wa Kifungu cha 42(7) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Chaguzi) Na. 4/79, Wasimamizi wa Uchaguzi walibandika fomu za uteuzi mahali pa wazi nje ya ofisi za Kata ili kuwapa nafasi Wagombea, Wasimamizi wa Uchaguzi na Mkurugenzi wa Uchaguzi watoe pingamizi dhidi ya wagombea kama wanazo.

4.3.1 Pingamizi zilitolewa kwa baadhi ya wagombea. Wasimamizi wa Uchaguzi walitoa uamuzi kuhusu pingamizi hizo, na wagombea ambao hawakukubaliana na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi walikata rufaa Tume chini ya Kifungu cha 44(5) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Chaguzi) Na. 4/79.

4.3.2 Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipokea jumla ya rufani hamsini na saba (57). Tume ilisikiliza rufani zote na rufani arobaini na mbili (42) zilionekana kuwa hazina msingi wowote, na kumi na tano (15) zilikubaliwa.

4.3.3 Kutokana na tatizo la mawasiliano kati ya Wasimamizi wa Uchaguzi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, baadhi ya rufani zilichelewa kuifikia Tume na hivyo kuathiri zoezi la upigaji kura. Kwa mfano rufani za Kata za Cheyo, Ng'ambo na Kitete (Halmashauri ya Manispaa ya Tabora) na Sultani Area (Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro) zilichelewa kutolewa uamuzi na hivyo zikailazimu Tume kupanga tarehe nyingine ya uchaguzi katika Kata hizo.

4.3.4 Tume ilikuwa inasikiliza rufaa bila ya waomba rufaa kuwepo isipokuwa pale ambapo iliona kuna haja ya kumwita muomba rufaa kutokana na ugumu wa maelezo ya rufaa au maelezo kutoeleweka vizuri au pale muomba rufaa anapoiomba Tume kutoa maelezo ya ziada, au mlalamikiwa anapoomba kujitetea.

4.3.5 Katika uchaguzi huo wa Kata ya Kariakoo, mgombea wa CCM kiti cha udiwani, alitoa pingamizi dhidi ya wagombea wengine wa kiti cha udiwani Kata ya Kariakoo, (Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam) wa UDP, TADEA

na PONA. Sababu za pingamizi zilikuwa kwamba wagombea hao wa UDP, TADEA na PONA walikuwa wamedhaminiwa na wapiga kura ambao si wakazi wa Kariakoo na hawajalipa kodi. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa Kata ya Kariakoo alikubali pingamizi hizo. Kwa kuwa wagombea hawakukubaliana na uamuzi huo, walikata rufaa kwa Tume. Maelezo yaliyokuwa mbele ya Tume yalikuwa hayatoshelezi hivyo Tume iliamua kuita waomba rufaa kutoa maelezo zaidi na kuwaleta watu waliowadhamini. Vile vile mgombea wa CCM aliomba kutoa maelezo zaidi kuhusiana na pingamizi yake aliyoitoa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Kata ya Kariakoo.

4.3.6 Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa Kata ya Kariakoo alikubali pingamizi hizo.

4.3.7 Baada ya waomba rufaa wote na aliyetoa pingamizi kutoa maelezo yao mbele ya kikao cha Tume, aliteuliwa Afisa mmoja wa Tume kufuatilia makazi ya wadhamini waliolalamikiwa ambaye alitoa taarifa yake baadae kwa Tume.

4.3.8 Baada ya Tume kusikiliza na kuzichunguza pingamizi hizi, uamuzi wake ulikuwa kama ifuatavyo:-

(a) Mgombea wa UDP alionekana kuwa ana sifa zilizotakiwa, yaani alilipa kodi na wadhamini wake wote walikuwa wakazi wa Kariakoo. Hivyo alikubaliwa kugombea;

(b) Mgombea wa PONA alishindwa kutoa ushahidi kuwa amelipa kodi ya maendeleo. Hivyo Tume ilithibitisha uamuzi wa Msimamizi Msaidizi kuwa mgombea wa PONA hastahili kugombea; na

(c) Mgombea wa TADEA alionekana kuwa hakulipa kodi za maendeleo za mwaka 1993 na 1994 wakati anawasilisha fomu zake za uteuzi tarehe 14 Agosti, 1994. Alilipa kodi tarehe 15 Agosti, 1994, baada ya siku ya uteuzi. Mgombea huyo alizuiwa kugombea kwa kukosa sifa.

## 4.4 KAMPENI ZA UCHAGUZI

4.4.1 Kipindi cha kampeni hutoa nafasi kwa vyama vya siasa pamoja na wagombea kuwasiliana rasmi na wapiga kura ili kuomba kura zao. Mara nyingi vyama vinapata nafasi wakati wa kampeni za uchaguzi ya kutangaza sera zao kwa wananchi ili wagombea wao waweze kuchaguliwa.

4.4.2 Kulingana na Kifungu cha 53(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Chaguzi) Tume inatakiwa ipange kipindi rasmi cha kampeni katika Uchaguzi wa

Madiwani. Tume ilitangaza kipindi cha kampeni kuanza tarehe 16 Oktoba hadi 29 Oktoba, 1994.

4.4.3 Chini ya Kifungu cha 53(3)(a), (b) na (c) vya Sheria Na. 4/79 kila mgombea, au chama cha siasa cha mgombea au mwakilishi wa mgombea alitakiwa kuandaa ratiba ya mikutano ya kampeni na kuiwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi. Msimamizi wa Uchaguzi alitakiwa kuzikagua na kuwashauri wagombea kufanya marekebisho pale inapobidi ili kuzuia kutokea migongano. Msimamizi wa Uchaguzi alitakiwa kupeleka ratiba ya kampeni kwa Mkuu wa Wilaya kwa taarifa na ili atoe ulinzi kwenye mikutano hiyo ya kampeni.

4.4.4 Kwa mujibu wa Kifungu 53(2) cha Sheria Na. 4/79, baada ya Tume kutangaza kipindi maalum cha kampeni na Msimamizi wa Uchaguzi kutoa nakala ya ratiba kwa Mkuu wa Wilaya, wagombea au vyama vya siasa au wawakilishi wa wagombea hawakutakiwa kuomba kibali cha kufanya mikutano ya hadhara kwa ajili ya kampeni.

4.4.5 Tukio moja kubwa lililotokea wakati wa kampeni ni lile la baadhi ya viongozi wa Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar wakiwa wanachama wa CCM kumsaidia mgombea wa CCM Kata ya Kariakoo, kupiga kampeni katika uchaguzi huo. Viongozi hao walitoa maneno ya kashfa kama vile mgombea wa UDP "alikuwa kama kicheche" na "hamheshimu baba yake". Maneno haya yalisababisha kesi ya Uchaguzi kufunguliwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na matokeo ya uchaguzi huo kutenguliwa. Mgombea wa CCM alikata rufaa Mahakama Kuu ambayo ilitoa uamuzi wake ambao hakuridhika nao. Aliomba rufaa Mahakama ya Rufaa lakini Halmashauri ya Jiji ilivunjwa kabla ya uamuzi wa Mahakama ya rufaa haujatolewa.

Hivyo Kata ya Kariakoo ilikaa bila Diwani tokea matokeo ya uchaguzi yalipotenguliwa na mahakama mpaka Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilipovunjwa na Waziri Mkuu na kuundwa Tume ya Jiji.

4.4.6 Kama ilivyokwisha kuelezwa, Kata zilizofanya kampeni ni 1,201 kati ya Kata 2,411. Wagombea wa Kata 1,210 hawakufanya kampeni kwa sababu walipita bila kupingwa.

4.4.7 Kutokana na mapendekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Serikali ilikubali kimsingi kutoa ruzuku, Shs. 30,000/= kwa kila mgombea kwa ajili ya kufidia sehemu ya gharama za kampeni za wagombea udiwani. Ruzuku hiyo ilitolewa kupitia makao makuu ya vyama.

4.4.8 Ruzuku hiyo ilitolewa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ya Shs. 10,000/= ilitolewa kwa kila mgombea wakati kampeni zinaendelea. Awamu ya pili ya Shs. 20,000/= ilitolewa baada ya uchaguzi.

4.4.9 Ruzuku hiyo ya Shs. 15,000/= ilitolewa kwa wagombea waliopita bila kupingwa. Ruzuku hi ilitolewa na Serikali kinyume cha mapendekezo ya Tume kuwa wagombea waliopita bila kupingwa wasipate ruzuku.

4.4.10 Ruzuku iliyotajwa hapo juu ilichelewa sana kutolewa na Hazina. Hali hiyo ilisababisha malalamiko mengi kwa Tume kutoka kwa vyama vya siasa na wagombea wao.

4.4.11 Baada ya Uchaguzi wa Madiwani kukamilika Serikali ilitoa ruzuku ya Shs. 100,000/= kwa kila Diwani aliyeshinda ili kumwezesha kuendesha shughuli za chama chake cha siasa katika Kata yake aliyoshinda. Kitendo hicho cha kutoa ruzuku hiyo kilizua malalamiko toka kwa vyama vya siasa na wahisani kwamba Tume inatumiwa na Serikali kukipendelea chama cha CCM ambacho ndicho kilichokuwa na madiwani wengi.

4.4.12 Tatizo kubwa lililojitokeza wakati wa kipindi cha kampeni ni kuwa baadhi ya wagombea na vyama vyao vya siasa hawakuzingatia ratiba zao za mikutano ya kampeni pamoja na kwamba waliziwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi na nakala kutolewa kwa Wakuu wa Wilaya. Hii ilisababisha usumbufu mkubwa kwa Polisi wa kulinda amani kwenye mikutano hiyo na wananchi waliotakiwa kuhudhuria mikutano hiyo, hivyo kuwakatisha tamaa wananchi hao.

## 4.5 UPIGAJI KURA

4.5.1 Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilipanga tarehe 30 Oktoba, 1994, kuwa siku ya Uchaguzi wa Madiwani na kutangaza tarehe hiyo kwenye Gazeti la Serikali Na. 460, la tarehe 5 Agosti, 1994.

4.5.2 Tarehe 29 Oktoba, 1994, siku iliyotangulia tarehe ya upigaji kura, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe. Jaji Lewis M. Makame, alitoa Tamko kwa wananchi wote wa Tanzania Bara juu ya Uchaguzi wa Madiwani. Aliwaomba wananchi wote walioandikishwa wajitokeze kwenda kupiga kura siku ya tarehe 30 Oktoba, 1994 (Tazama Kiambatisho Na. 5).

4.5.3 Kwa mujibu wa Kifungu cha 58 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Chaguzi) Na. 4/79, kila mgombea alikuwa na haki ya kuteua wakala wa upigaji kura mmoja

kwa kila kituo cha kupigia kura. Tume iliwagharamia mawakala hao kwa kuwalipa posho siku za semina na siku ya upigaji kura.

4.5.4 Upigaji kura ulifanyika kwenye Kata 1,201 tu katika Halmashauri 94. Kata nyingine za Halmashauri hizo na za Halmashauri 8 za Monduli, Makete, Korogwe, Ngorongoro, Simanjiro, Chunya, Mafia na Liwale upigaji kura haukufanyika kwa sababu wagombea udiwani wa Kata hizo hawakuwa na wapinzani.

4.5.5 Kutokana na sababu mbalimbali, baadhi ya Kata hazikufanya uchaguzi tarehe 30 Oktoba, 1994, kama ifuatavyo:-

(a) Katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Kata za Kitete, Cheyo na Ng'ambo hazikufanya uchaguzi kwa sababu ratiba ya uchaguzi iliathiriwa na rufani za wagombea.

(b) Uchaguzi ulisimamishwa katika Kata ya Njoro (Halmashauri ya Wilaya ya Same) kutokana na mgombea wa CCM kufariki kabla ya siku ya uchaguzi.

(c) Kata ya Lumbila katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa hakukuwa na mgombea aliyerudisha fomu na kuteuliwa na Msimamizi wa uchaguzi siku ya uteuzi.

(d) Kata ya Madope katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa mgombea wa CCM aliyekuwa amepita bila kupingwa alifariki tarehe 24 Septemba, 1994.

(e) Kata ya Wampembe katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkansi hakukuwa na wagombea kwa sababu hawakurudisha fomu siku ya uteuzi na hivyo uteuzi haukufanyika.

(f) Katika Kata ya Melela (Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro) mgombea alifariki siku moja kabla ya upigaji kura.

(g) Kata ya Kigamboni katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam uchaguzi ulisimamishwa kwa amri ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kivukoni kufuatia malalamiko ya baadhi ya wanachama wa CCM kwamba katika uteuzi wa wagombea uliofanywa ndani ya CCM haki haikutendeka. Uchaguzi mpya ulifanyika baada ya Mahakama Kuu kutengua uamuzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi.

(h) Kata ya Sultani Area katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, ratiba ya uchaguzi iliathiriwa na rufani za wagombea.

(i) Kata ya Nyakatende katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, uchaguzi ulisimamishwa kwa amri ya Mahakama ya Hakimu Mkazi kufuatia malalamiko ya baadhi ya wanachama wa CCM kwamba katika uteuzi wa wagombea ndani ya CCM haki haikutendeka.

Uchaguzi mpya katika Kata hizo ulifanyika kama ifuatavyo:-

(a) Tarehe 6 Novemba, 1994 - Kata za Kitete, Cheyo, Ng'ambo na Sultan Area;
(b) Tarehe 8 Januari, 1995 - Kata ya Njoro;
(c) Tarehe 29 Januari, 1995 - Kata ya Wampembe;
(d) Tarehe 12 Februari, 1995 - Kata za Melela na Kigamboni; na
(e) Tarehe 21 Mei, 1995 - Kata za Lumbila na Madope.

## 4.6 MATOKEO YA UCHAGUZI

4.6.1 Msimamizi wa Uchaguzi ndiye mwenye mamlaka ya kuhesabu kura na kutangaza matokeo. Kwa Uchaguzi wa Madiwani wa mwaka 1994, kura zilihesabiwa tarehe 31 Oktoba, 1994, kwenye makao makuu ya kila Kata. Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi walihusika na zoezi hilo kwa kusaidiana na wahesabu kura (enumerators) waliowateua.

4.6.2 Kila mgombea alitakiwa kuteua wakala wa kuhesabu kura mmoja kushuhudia zoezi la kuhesabu kura Makao Makuu ya Kata.

4.6.3 Matokeo ya Uchaguzi wa Madiwani kwa Kata 1,201 zilizofanya uchaguzi yalikuwa kama ifuatavyo:-

| Chama | Viti vya Udiwani |
|---|---|
| CCM | 1,124 |
| CHADEMA | 22 |
| CUF | 21 |
| UDP | 15 |
| NCCR-MAGEUZI | 14 |
| UMD | 3 |
| TADEA | 2 |
| | 1,201 |

4.6.4 Kwa mujibu wa Kifungu cha 45(2) cha Sheria Na. 4 ya 1979, wagombea udiwani wa Kata 1,210 waliokuwa hawana wapinzani walitangazwa kuwa wamechaguliwa kuwa madiwani wa Kata hizo. Vyama vilivyohusika ni kama ifuatavyo:-

| Chama | Viti vya Udiwani |
|---|---|
| CCM | 1,208 |
| NCCR-MAGEUZI | 1 |
| UDP | 1 |
| | 1,210 |

4.6.5 Kwa mujibu wa Vifungu vya 35(1)(d) na 19(1)(c) vya Sheria Na. 7 ya 1982, na Sheria Na. 8 ya 1982, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliteua madiwani wa viti maalum vya wanawake visivyopungua 25% ya madiwani wa kuchaguliwa, kwa kila Halmashauri. Tume iliandaa Kanuni zilizotumika katika uteuzi huo (Tazama Kiambatisho Na. 6).

4.6.6 Madiwani wa viti maalum vya wanawake walioteuliwa walikuwa 652 kama ifuatavyo:-

| Chama | Viti vya Madiwani Wanawake |
|---|---|
| CCM | 633 |
| CUF | 8 |
| CHADEMA | 5 |
| NCCR-MAGEUZI | 3 |
| UDP | 2 |
| | 652 |

4.6.7 Katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda waliteuliwa madiwani wanawake watano (5). Kati ya hao, CCM ilipata madiwani wanne (4), nafasi moja (1) ya udiwani ilikuwa ni kwa vyama vitatu, UMD, UDP na CUF ambavyo kila kimoja kilishinda kiti kimoja cha udiwani katika uchaguzi. Kwa vile isingewezekana kukigawa kiti hicho, Tume ilivishauri vyama hivyo vikutane na kukubaliana chama kipi kipate kiti hicho. Vyama hivyo vilikubaliana kuwa CUF ipewe kiti hicho.

4.6.8 Baada ya matokeo ya uchaguzi na uteuzi wa madiwani wa viti maalum vya wanawake Tanzania Bara ilikuwa na jumla ya madiwani 3,063 kama ifuatavyo:-

| Chama | Viti vya Udiwani |
|---|---|
| CCM | 2,965 |
| CUF | 29 |
| CHADEMA | 27 |
| UDP | 19 |
| NCCR-MAGEUZI | 18 |
| UMD | 3 |
| TADEA | 2 |
| | 3,063 |

# 5. HITIMISHO

5.1 Taarifa hii imeeleza kwa ufupi juu ya Uchaguzi wa Madiwani wa mwaka 1994. Uchaguzi huo ulikuwa wa kwanza wa madiwani kufanyika katika mfumo wa vyama vingi vya siasa tangu kurejeshwa kwa mfumo huo mwaka 1992.

5.2 Halmashauri 102 za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji zenye jumla ya Kata 2,411 zilihusika kwenye Uchaguzi wa Madiwani (Tazama Kiambatisho Na. 7).

5.3 Vyama vya siasa kumi na vitatu (13) vilivyopata usajili kamili vilishiriki uchaguzi huo. Kama inavyoonekana katika sura zilizotangulia, idadi kubwa ya vyama havikuteua wagombea katika baadhi ya Kata, hali ambayo ilisababisha wagombea udiwani wengi kupita bila kupingwa. Ilionekana wazi katika uchaguzi kwamba baadhi ya vyama havikuwa vimeenea au kujijenga katika Kata za maeneo ya vijijini.

5.4 Uchaguzi huo uliiongezea Tume uzoefu wa uendeshaji uchaguzi na kuweza kupanga mipango ya kuendesha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995. Kwa mfano, kufuatia ziara za wajumbe wa Tume mikoani wakati wa Uchaguzi wa Madiwani, Tume ilibaini kuwa baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya walikuwa wakiingilia shughuli za uchaguzi. Kutokana na tatizo hilo, Tume katika kikao chake Na. 8/1994 cha tarehe 4 Novemba, 1994, kiliamua kuwa kwa uchaguzi ujao wa Rais na Wabunge Tume ichukue jukumu la kuwaelimisha viongozi wa vyama vya siasa na Serikali wakiwemo Wakuu wa Mikoa na Wilaya, uamuzi ambao ulitekelezwa wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995.

5.5 Pamoja na matatizo yaliyoikabili Tume kama vile ukosefu wa ofisi, upungufu wa watumishi na uhaba wa vitendea kazi, Tume iliendesha uchaguzi huo kwa ufanisi na mafanikio makubwa.

5.6 Uchaguzi wa Madiwani wa mwaka 1994, ulifanyika katika hali ya utulivu na amani. Tume inaamini kwamba matokeo ya uchaguzi huo yanaonyesha wazi matakwa halisi ya wapiga kura.

KIAMBATISHO NA. 1

## MPANGO WA UTEKELEZAJI

| | | JUNI | | | | JULAI | | | | AGOSTI | | | | SEPT. | | | | OKTOBA | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 | 1 | 2 | 3 | 4 |
| 1 | Warsha ya Waandishi - 11 - 17/6/94 | | ■ | ■ | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 2 | Uteuzi Rasmi wa Wasimamizi wa Uchaguzi | | ■ | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 3 | Makisio ya Wapiga Kura, na Vituo vya Kupigia Kura | ■ | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 4 | Warsha ya Mafunzo kwa Wakufunzi 19-23/6/94 | | | | ■ | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 5 | Semina kwa Wasimamizi wa Uchaguzi 27/6 - 2/7/94 | | | | ■ | ■ | | | | | | | | | | | | | | | |
| 6 | Usambazaji wa Vifaa kwa ajili ya uandikishaji na Uteuzi (Kutoka Tume kwenda kwa Wasimamizi wa Uchaguzi) | | | ■ | ■ | ■ | ■ | | | | | | | | | | | | | | |
| 7 | Semina kwa Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi | | | | | ■ | ■ | | | | | | | | | | | | | | |
| 8 | Usambazaji wa vifaa vya uandikishaji kutoka kwa Wasimamizi wa Uchaguzi kwenda kwenye Kata | | | | | | | ■ | | | | | | | | | | | | | |
| 9 | Utayarishaji wa vituo vya kuandikisha wapiga kura | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | ■ | | | | | | | | | | | | | |
| 10 | Uteuzi wa Waandishi Wasaidizi na semina kwa ajili yao | | | | | ■ | ■ | ■ | | | | | | | | | | | | | |
| 11 | Utumaji wa fedha kutoka Tume kwenda kwa Wasimamizi wa Uchaguzi | | | | ■ | ■ | ■ | | | | | | | | | | | | | | |
| 12 | Uandikishaji wa wapiga kura 1-14/8/94 | | | | | | | | | ■ | ■ | | | | | | | | | | |
| 13 | Uteuzi wa wagombea 7/8/94 | | | | | | | | | | ■ | | | | | | | | | | |
| 14 | Pingamizi dhidi ya uteuzi 8/8/94 | | | | | | | | | | ■ | | | | | | | | | | |
| 15 | Kampeni za uchaguzi 16-29/10/94 | | | | | | | | | | | | | | | | | | ■ | ■ | ■ |
| 16 | Semina kwa Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wavituo vya kupigia kura 27 - 29/10/94 | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | ■ |
| 17 | Siku ya kupiga kura 30/10/94 | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | ■ |

# MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA, 1994

| NA | MAELEZO YA SHUGHULI | TAREHE YA UTEKELEZAJI | MTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 1 | (a) Kusambaza fomu za uteuzi (Na. 2, 3 na 13) kwa vyama | 16/8 - 31/8/94 | Tume |
| | (b) Uteuzi wa wagombea wanawake (viti maalum) | Kabla ya 10/10/94 | Vyama vya siasa |
| 2 | Usambazaji na Utoaji wa Fedha kwa Wasimamizi wa Uchaguzi (Fedha kwa ajili ya shughuli za uandikishaji) | 2/8 - 4/8/94 | Tume kushirikiana na BOT/NBC |
| 3 | Mawasiliano na Wizara ya Fedha (HAZINA) kwa ajili ya utoaji wa fedha awamu ya pili (kiasi kilichobaki). | *Immediately* | Tume |
| 4 | Usambazaji wa vifaa vya elimu ya uchaguzi kwa umma kwenye Halmashauri (awamu ya kwanza) | 4/8 - 13/8/94 | Tume |
| 5 | (a) Siku ya uteuzi<br>(b) Pingamizi dhidi ya wagombea walioteuliwa | 14/8/94<br>15/8/94 | Wasimamizi wa Uchaguzi |
| 6 | Kusambazwa kwa Wasimamizi wa Uchaguzi wote orodha ya vyama vyote vilivyopata usajili kamili na anwani zao | 5/8/94 | Tume |
| 7 | Kufuatilia maamuzi yote ya Serikali kuhusu ushiriki wa vyama vya siasa kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, 1994 katika Kata | 5/8 - 31/8/94 | Tume/Wasimamizi wa Uchaguzi |
| 8 | Uchapishaji wa nakala 15,000 za rasimu kwa madhumuni ya uchapishaji wa:-<br>(a) Mfano wa karatasi za kura<br>(b) Karatasi za kura<br>(c) karatasi za kura bubu | 10/8 - 15/8/94 | Tume |
| 9 | Kutangaza katika Gazeti la Serikali Siku ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa | 5/8/94 | Tume/Mpiga Chapa wa Serikali |
| 10 | Uchapishaji wa Maelekezo kwa Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo vya Upigaji Kura | 16/8 - 31/8/94 | Tume |
| 11 | Ufuatiliaji wa uandikishai wa wapiga kura kutoka Halmashauri mbalimbali | 16/8 - 5/9/94 | Tume |
| 12 | Kusambaza kwa Wasimamizi wa Uchaguzi mfano wa Hati ya Uchaguzi (Certificate of Election) | 21/8 - 31/8/94 | Tume |
| 13 | Kutayarisha na kusambaza kwa Wasimamizi wa Uchaguzi, mfano wa kura zitakazokubaliwa na mfano wa kura zitakazokataliwa wakati wa uchaguzi wa 30/10/94 | 31/8/94 - 10/9/94 | Tume |
| 14 | Mpango wa kupata masanduku ya kura mapya 13,000 | 9/8 - 298/94 | Tume |

| NA | MAELEZO YA SHUGHULI | TAREHE YA UTEKELEZAJI | MTEKELEZJI |
|---|---|---|---|
| 15 | Mpango wa upakaji rangi (nyeusi) masanduku ya kura 15,000 | 11/8 - 30/8/94 | Tume |
| 16 | Upatikanaji wa mishumaa 35,000 | kabla ya 15/9/94 | Tume |
| 17 | Utayarishaji wa rasimu za karatasi za kura na mfano wa karatasi za kura kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika tarehe 30/10/94 | 16/8 - 29/8/94 | Tume |
| 18 | Uchapishaji wa karatsi za kura na mfano wa Karatasi za Kura Bubu | 1/9 - 30/9/94 | Tume |
| 19 | Uchapishaji wa Mfano wa Karatasi za Kura na Kura Maalum | 1/9 - 30/9/94 | Tume/ODA |
| 20 | Semina kwa viongozi wa vyama vya siasa na Wakurugenzi wa Halmashauri | | Tume |
| 21 | Matangazo kwa ajili ya Elimu ya Uchaguzi kwa Umma kuhusu demokrasia ya vyama vingi kwa ajili ya uchaguzi wa madiwani | | Tume |
| 22 | Utengenezaji na uagizaji wa marobota 120 ya kanga, @ 285,000/= | | Tume/Urafiki Textiles |
| 23 | Kuagiza na kutengeneza T-Shirts 7,200 @ kugharimu Shs. 834/= | | Tume/Sunflag - Arusha |
| 24 | Utengenezaji na uagizaji wa *stickers* 15,000, @ kugharimu Shs. 210/= jumla Shs. 3,150,000/= | Siku 21 kuanzia tarehe 16/8/94 | Tume |
| 25 | Utayarishaji wa makisio ya awamu ya tatu ya fedha kwa ajili ya uchaguzi wa madiwani wa Kata, na baadaye kupeleka fedha kwenye Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispa | 16/8 - 26/8/94 | Tume |
| 26 | Usambazaji wa mfano wa karatasi za kura na vifaa vingine vya uchaguzi kwenye Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa | 24/9 - 8/10/94 | Tume |
| 27 | Kampeni kwa ajili ya wagombea wa udiwani | 16/10 - 29/10/94 | Wagombea/Vyama vya siasa |
| 28 | Semina kwa ajili ya Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo vya Kura na Mawakala wa Upigaji Kura | 27/10 - 28/10/94 | Wasimamizi wa Uchaguzi |
| 29 | Kupeleka Wasimamizi na Wasimamizi Wasaidizi wa Vituo vya Kura pamoja na vifaa vya uchaguzi kwenye vituo vya upigaji kura | 29/10/94 | Tume |
| 30 | Siku ya Upigaji Kura | 30/10/94 | Wapiga kura |
| 31 | Kuhesabu Kura na Kutangaza Matokeo | 31/10/94 | Tume |

## MAKADIRIO YA MATUMIZI YA UCHAGUZI WA MADIWANI, 1994 (REKEBISHO NA. 4) OKTOBA, 1994

| MAELEZO | | JUMLA YA MAKADIRIO | FEDHA KUTOKA HAZINA | MCHANGO WA KUNDI LA WAHISANI | MCHANGO WA SERIKALI YA UINGEREZA |
|---|---|---|---|---|---|
| A: | UANDIKISHAJI | 1,346,112,100/= | 1,346,112,100/= | - | - |
| B: | UTEUZI | 19,171,300/= | 19,171,300/= | - | - |
| C: | KARATASI ZA KURA | 978,344,440/= | - | 407,209,765/= | 571,134,675/= |
| D: | MAFUNZO | 3,650,391,700/= | 1,714,844,020/= | 1,935,547,680/= | - |
| E: | MAANDALIZI YA VITUO VYA KUPIGIA KURA | 364,082,760/= | 335,582,760/= | 28,500,000/= | - |
| F: | KAMPENI | 77,519,600/= | 49,019,600/= | 28,500,000/= | - |
| G: | SIKU YA UPIGAJI KURA | 1,937,200,400/= | 716,682,120/= | 1,220,518,280/= | - |
| H: | KUHESABU KURA | 159,340,400/= | 159,340,400/= | - | - |
| I: | TUME-MAKAO MAKUU | 51,242,700/= | 51,242,700/= | - | - |
| J: | ELIMU KWA UMMA | 470,217,000/= | 8,005,000/= | 462,212,000/= | - |
| K: | UHASIBU NA UKAGUZI | 20,000,000/= | - | 20,000,000/= | - |
| JUMLA | | 9,053,622,400/= | 4,400,000,000/= | 4,082,487,725/= | 571,134,675/= |
| DHARURA | | XX | XX | XX | |
| JUMLA KUU | | 9,053,622,400/= | 4,400,000,000/= | 4,082,487,725/= | 571,134,675/= |

**KIAMBATISHO NA. 3**

## MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA UCHAGUZI ZILIZOTOLEWA NA WAHISANI MBALIMBALI

| NO | JINA LA NCHI AU TAASISI | KIASI | MAELEZO YA MATUMIZI |
|---|---|---|---|
| 1. | MAREKANI (USAID) | 11,700,000/= | Uchapishaji wa vipeperushi (leaflets) |
| 2. | KUNDI LA WAHISANI (GROUP OF DONORS) i.e. DENMARK, SWEDEN, NA JUMUIYA YA NCHI ZA ULAYA (E.E.C.) | 2,888,803,516/= | Uchapishaji wa vifaa vya Elimu kwa wapiga kura, yaani kanga, T-Shirts, mabango, vipeperushi na Maelekezo kwa Wasimamizi wa Uchaguzi, Waandishi Wasaidizi, Wasimamizi wa Vituo vya Kura, Vyama vya Siasa na Wagombea na Mpiga Kura<br><br>Usafirishaji wa vifaa vya uchaguzi<br><br>Kugharamia semina za wasimamizi wa vituo, Wasimamizi wasaidizi wa vituo na mawakala katika jiji la Dar es Salaam<br><br>Ununuzi wa wino usiofutika<br><br>Gharama za siku ya kupiga kura |
| 3. | UINGEREZA (UK) | 571,200,000/= | Uchapishaji wa karatasi za kura, mfano wa kura, kura bubu na kura maalum |
| JUMLA | | 3,471,703,516/= | |

# ORODHA YA VIFAA VILIVYOTUMIKA KATIKA UCHAGUZI WA MADIWANI

## VIFAA VYA UANDIKISHAJI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Fomu Na. 1 | - | Ombi la Kujiandikisha Kuwa Mpiga kura/taarifa ya kubadilisha Habari za Kujiandikisha. |
| 2. | Fomu Na. 7 | - | Daftari ya Wapiga Kura Walioandikishwa. |
| 3. | Fomu Na. 8 | - | Tamko la Kisheria kwa Kupotea au Kuharibika kwa Shahada ya Kuandikishwa. |
| 4. | Fomu Na. 9 | - | Maelezo ya Kukataa Kuandikisha. |

5. Carbon Papers.
6. Kalamu za Wino.
7. "Bango" la Kituo cha Kuandikisha Wapiga Kura.
8. "Drawing pins".
9. Kidawati cha Wino (Stamp Pad)
10. Chupa ya Wino (Stamp Pad Ink).

## VIFAA VYA MTU ANAYEOMBA KUGOMBEA NAFASI YA UDIWANI

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11. | Fomu Na. 2 | - | Karatasi ya Uteuzi. |
| 12. | Fomu Na. 3 | - | Tamko la Kisheria la Mgombea Uchaguzi wa Udiwani. |
| 13. | Fomu Na. 13 | - | Maelezo Binafsi ya Mtu Anayeomba Nafasi ya Kugombea Udiwani. |

## VIFAA VYA WAKATI WA KUPIGA KURA

1. Bahasha la Kituo (Orodha ya Vifaa kwa Kila Kituo Kimoja cha Kura).
2. Karatasi za Kura.
3. Karatasi za Kura Bubu.
4. Wembe*.
5. Tamko (Fomu Na. 4)*.
6. Hesabu ya Karatasi za Kura (Fomu Na. 6)*.
7. Taarifa ya Msimamizi wa Kituo cha Kura (Fomu Na. 5)*.
8. Maelezo na Hadhari kwa Wapiga Kura*.
9. Bahasha ya Karatasi za Kura (Na. 1)*.
10. Bahasha ya Vibutu vya Karatasi za Kura Zilizotumika (Na. 2)*.
11. Bahasha ya Karatasi za Kura Ambazo Hazikutumika na Zilizoharibika (Na. 3)*.
12. Bahasha ya Daftari ya Orodha ya Wapiga Kura na Shahada za Utumishi (Na. 4)*.
13. Bahasha ya Kura Bubu (Na. 5)*.
14. Bahasha ya Orodha ya Kura Bubu (Na. 6)*.
15. Bango la "Kituo cha Kupigia Kura"*.
16. Utepe wa Gundi*.
17. Utepe wa Kamba*.
18. Drawing Pins*.
19. Mfano wa karatasi ya kura.
20. Kibiriti*.
21. Lakiri (Sealing Wax)*.

22. Kalamu za Wino.
23. Kijitabu cha Karatasi za Kuandikia*.
24. Maelekezo kwa Wasimamizi wa Vituo vya Kura*.
25. Karatasi za Kukaushia Wino*.
26. Mshumaa*.
27. Mhuri wa Mpira wa Kituo cha Kura.
28. Mhuri wa Shaba.
29. Kidawati cha Wino.
30. Chupa ya Wino (Stamp Pad Ink).
31. Chupa ya Wino Usiofutika.
32. Kufuli la Sanduku la Kura.
33. Sanduku la Kura.
34. Rubber Bands*.
35. Fomu ya Kiapo cha Kutunza Siri.
36. Bahasha - "Kura"*.
37. Fomu Na. 10 - Hesabu za Kura*.
38. Fomu Na. 11 - Maelezo ya Karatasi za Kura*.
39. Fomu Na. 12 - Uthibitisho wa Karatasi za Kura*.
40. Fomu CF. 3 - Malalamiko au Ridhaa ya Wakili wa Upigaji Kura Kabla ya Kuanza Upigaji Kura*.
41. Fomu CF. 4 - Malalamiko ya Mpiga Kura Kuhusu Mwenendo wa Upigaji Kura Katika Kituo/Eneo la Upigaji Kura*.
42. Fomu CF. 5 - Malalamiko au Ridhaa ya Wakili wa Upigaji Kura Baada ya Kukamilika Upigaji Kura Kituoni*.
43. Fomu RF. 1 - Taarifa ya Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura*.

<u>FOMU ZA MALALAMIKO AU RIDHAA YA WAKILI WA KUHESABU KURA KATIKA HATUA MBALIMBALI ZA KUHESABU KURA KITUONI (FOMU NA. 6 NA NA. 7)</u>

44. Fomu CF. 6 - Malalamiko au Ridhaa ya Wagombea Kabla ya Kuanza kwa Utaratibu wa Kuhesabu Kura.
45. Fomu CF. 7 - Malalamiko au Ridhaa ya Mgombea au Wakili Katika Hatua za Kuhesabu Kura.
46. Taarifa ya Msimamizi wa Uchaguzi kwa Mgombea Udiwani aliyeshinda, kumwarifu kwa maandishi kuhusu kuchaguliwa kwake kuwa Diwani wa Kata inayohusika ambayo iko katika Halmashauri inayohusika.
47. Taarifa ya Matokeo ya Uchaguzi wa Madiwani kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutoka kwa Msimamizi wa Uchaguzi.

**NB:** * Vifaa hivi huwekwa kwenye bahasha la kituo.

## TAMKO LA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI JUU YA UCHAGUZI WA MADIWANI

Ndugu wananchi wote wa Tanzania Bara, kesho, Jumapili tarehe 30 Oktoba, mwaka huu, ndio siku ambayo tukiisubiri kwa hamu. Kesho ndio siku ya Uchaguzi wa Madiwani. Uchaguzi wa kesho ni tofauti na chaguzi za madiwani zilizopita. Kwa mara ya kwanza kesho kutakuwepo na wagombea viti vya udiwani kutoka vyama vingi vya siasa.

Kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, ninawaomba wale wananchi wote waliojiandikisha kwenda kwenye vituo vyao kupiga kura. Katika juma mbili zilizopita wagombea wamekuwa wakijieleza nini kila mmoja wao anachokusudia kukifanya katika Kata yake kama atachaguliwa. Kesho ndio siku ya kuhakikisha kuwa unampata diwani umtakae na unayeamini kuwa ataisaidia Kata yako.

Kura yako ni siri yako. Hakuna hata mtu mmoja atakayeweza kujua umepigaje kura yako. Hivyo usiwe na hofu hata chembe kupiga kura utakavyo. Huenda akawepo Polisi hapo kituoni. Usimuogope. Yeye yupo hapo kudumisha amani. Hayupo hapo kukutisha.

Watanzania tunatambuliwa kwa sifa ya amani na utulivu. Ni tumaini letu kuwa kesho tutaiendeleza na kuidumisha sifa hii. Tunawaomba mfuate maagizo yote yatakayotolewa na Msimamizi wa Kituo na Wasaidizi wake. Subiri katika foleni kwa utulivu kungojea zamu yako ya kupiga kura. Ukiisha kupiga kura ondoka kituoni taratibu.

Nachukua nafasi hii kumtakia kila mmoja upigaji kura mwema na wa mafanikio hapo kesho.

(Jaji Lewis M. Makame)
**MWENYEKITI**
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**29 OKTOBA, 1994.**

## KANUNI ZINAZOHUSU UTEUZI WA MADIWANI WA VITI MAALUM VYA WANAWAKE

Sifa kwa viti maalum

10. (1) Mwanamke yeyote anayedhaminiwa na chama cha siasa aweza kugombea uteuzi wa udiwani katika Halmashauri ya Wilaya, Mji, Manispaa au Jiji chini ya sehemu hii.

(2) Bila kuathiri aya (1) ya Kanuni hii mwanamke atastahili kuteuliwa chini ya sehemu hii endapo ana sifa za kuchaguliwa kwa mujibu wa kifungu cha 39 cha sheria

Chama cha siasa kupendekeza mgombea

(3) Bila kuathiri aya (1) na (2) ya Kanuni hii mwanamke mwenye sifa chini ya sehemu hii hahitajiwi kudhaminiwa na mpiga kura yeyote.

11. (1) Kila chama cha siasa kitapewa fursa ya kupendekeza idadi yoyote ya wagombea wanawake kinayotaka kwa uteuzi wa viti maalum vya udiwani katika Halmashauri za Wilaya, Mji, Manispaa au Jiji.

Isipokuwa kwamba chama chochote cha siasa hakitapendekeza idadi ya wagombea inayozidi asilimia thelathini (30%) ya idadi ya viti vyote vya Udiwani vya Halmashauri inayohusika.

(2) Chama chochote cha siasa chaweza kupendekeza majina ya wagombea wanawake waliogombea Uchaguzi wa Madiwani.

(3) Kila pendekezo la uteuzi chini ya sehemu hii lifanywe katika hati ya kawaida ya uteuzi.

(4) Hati ya uteuzi iambatanishwe na picha nne zenye ukubwa wa postikadi za rangi nyeusi na nyeupe za mgombea mwanamke.

(5) Kila chama kinachodhamini kitaipelekea Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa ajili ya kila mgombea mwanamke kinayempendekeza hati za uteuzi pamoja na picha kama zilivyotajwa katika aya ya 3) ya Kanuni hii.

(6) Kila chama kinachodhamini kitaipelekea Tume ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na hati za uteuzi orodha ya wagombea wanawake kinachowadhamini kwa mpangilio wa upendeleo.

(7) Chini ya Kifungu (6) jina linaloorodheshwa kabla ya jingine litachukuliwa kwamba linapendelewa kuliko jina linalofuata katika orodha hiyo.

(8) Majina ya wagombea wanawake yatapelekwa kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kabla ya siku ya thelathini baada ya siku ya uteuzi kwa ajili ya Uchaguzi wa Madiwani.

Isipokuwa kwamba katika mazingira ya pekee Tume yaweza kwa hiari yake kuongeza muda wa kupokea jina la mgombea yeyote.

(9) Tume ya Taifa ta Uchaguzi itagawa idadi ya viti maalum vya wanawake kwa kila chama cha siasa katika Halmashauri kwa uwiano wa idadi ya wajumbe wa vyama vya siasa waliochaguliwa katika Halmashauri ambao Mamlaka ya Uchaguzi itakuwa imetangaza kuchaguliwa kwao katika Halmashauri.

12. Idadi ya viti maalum vya wagombea wanawake haitapungua asilimia ishirini na tano (25) ya wajumbe wote wa Halmashauri. Idadi ya viti maalum

Isipokuwa kwamba katika ugawaji wa viti maalum kwa Halmashauri na kwa kila chama cha siasa sehemu (fraction) ya namba isiyozidi nusu haitazingatiwa, lakini namba yenye sehemu (fraction) ya namba inayozidi nusu itafanywa kuwa namba kamili ya juu inayofuata.

13. Tume ya Taifa ya Uchaguzi itatangaza majina ya wagombea wanawake walioteuliwa kuchukua viti maalum katika kipindi kisichozidi siku kumi na nne baada ya kupokea matokeo ya uchaguzi, na itachapisha majina yao katika Gazeti la Serikali. Tangazo la uteuzi

## ORODHA YA HALMASHAURI ZOTE TANZANIA BARA ZILIZOHUSIKA NA UCHAGUZI WA MADIWANI, OKTOBA, 1994

### MKOA WA ARUSHA
1. Halmashauri ya Manispaa ya Arusha
2. Halmashauri ya Wilaya ya Babati
3. Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru
4. Halmashauri ya Wilaya ya Hanang
5. Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto
6. Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu
7. Halmashauri ya Wilaya ya Mondulu
8. Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro
9. Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro

### MKOA WA DAR ES SALAAM
10. Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam

### MKOA WA DODOMA
11. Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma
12. Halmashauri ya Wilaya ya Dodoma
13. Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa
14. Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa

### MKOA WA IRINGA
15. Halmashauri ya Manispaa ya Iringa
16. Halmashauri ya Wilaya ya Iringa
17. Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa
18. Halmashauri ya Wilaya ya Makete
19. Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi
20. Halmashauri ya Wilaya ya Njombe

### MKOA WA KAGERA
21. Halmashauri ya Mji wa Bukoba
22. Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba
23. Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo
24. Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe
25. Halmashauri ya Wilaya ya Muleba
26. Halmashauri ya Wilaya ya Ngara

### MKOA WA KIGOMA
27. Halmashauri ya Mji wa Kigoma/Ujiji
28. Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma
29. Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu
30. Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo

### MKOA WA KILIMANJARO
31. Halmashauri ya Manispaa ya Moshi
32. Halmashauri ya Wilaya ya Moshi
33. Halmashauri ya Wilaya ya Hai
34. Halmashauri ya Wilaya ya Rombo
35. Halmashauri ya Wilaya ya Same
36. Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga

### MKOA WA LINDI
37. Halmashauri ya Mji wa Lindi
38. Halmashauri ya Wilaya ya Lindi
39. Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea
40. Halmashauri ya Wilaya ya Liwale
41. Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa

### MKOA WA MARA
42. Halmashauri ya Mji wa Musoma
43. Halmashauri ya Wilaya ya Musoma
44. Halmashauri ya Wilaya ya Bunda
45. Halmashauri ya Wilaya ya Tarime
46. Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti

### MKOA WA MBEYA
47. Halmashauri ya Manispaa ya Mbeya
48. Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya
49. Halmashauri ya Wilaya ya Ileje
50. Halmashauri ya Wilaya ya Kyela
51. Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi
52. Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe
53. Halmashauri ya Wilaya ya Chunya

### MKOA WA MOROGORO
54. Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro
55. Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro
56. Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero
57. Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga
58. Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa

### MKOA WA MTWARA
59. Halmashauri ya Mji wa Mtwara/Mikindani
60. Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara
61. Halmashauri ya Wilaya ya Masasi
62. Halmashauri ya Wilaya ya Newala

MKOA WA MWANZA

63. Halmashauri ya Manispaa ya Mwanza
64. Halmashauri ya Wilaya ya Geita
65. Halmashauri ya Wilaya ya Magu
66. Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba
67. Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema
68. Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe

MKOA WA PWANI

69. Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha
70. Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo
71. Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe
72. Halmashauri ya Wilaya ya Mafia
73. Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji

MKOA WA RUKWA

74. Halmashauri ya Mji wa Sumbawanga
75. Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga
76. Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda
77. Halmashauri ya Wilaya ya Nkansi

MKOA WA RUVUMA

78. Halmashauri ya Mji wa Songea
79. Halmashauri ya Wilaya ya Songea
80. Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga
81. Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru

MKOA WA SHINYANGA

82. Halmashauri ya Mji wa Shinyanga
83. Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga
84. Halmashauri ya Wilaya ya Kahama
85. Halmashauri ya Wilaya ya Maswa
86. Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi
87. Halmashauri ya Wilaya ya Meatu

MKOA WA SINGIDA

88. Halmashauri ya Mji wa Singida
89. Halmashauri ya Wilaya ya Singida
90. Halmashauri ya Wilaya ya Iramba
91. Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni

MKOA WA TABORA

92. Halmashauri ya Manispaa ya Tabora
93. Halmashauri ya Wilaya ya Tabora
94. Halmashauri ya Wilaya ya Igunga
95. Halmashauri ya Wilaya ya Urambo
96. Halmashauri ya Wilaya ya Nzega

MKOA WA TANGA

97. Halmashauri ya Manispaa ya Tanga
98. Halmashauri ya Wilaya ya Pangani
99. Halmashauri ya Wilaya ya Handeni
100. Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe
101. Halmashauri ya Wilaya ya Muheza
102. Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto